



CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM  
NDAKI YA SAYANSI ZA JAMII

**MHADHARA WA UMMA**



**MUSTAKABALI WA MALIASILI  
NA HAKI ZA BINADAMU NCHINI  
TANZANIA**



**VSS2024**

## Mhadhiri: Prof. Emmanuel Sulle

**Chuo Kikuu cha Aga Khan,  
Tanzania**



### Muhtasari

Uhifadhi wa maliasili na haki za binadamu zina historia ndefu iliyogubikwa na migogoro barani Afrika. Hii ni kuanzia enzi za ukoloni ambapo mahitaji ya wenyeji waliotegemea misitu, wanyamapori na ardhi ya kilimo yalisimamiwa na sheria za kibaguzi za mamlaka za kikoloni. Kuna maoni kwamba historia hii mara nyingi imekuwa chimbuko la sera na maamuzi yanayosimamia maliasili yanayoleta migogoro na kuendelea kuwa kiini cha mijadala kuhusu uhusiano kati ya hifadhi za taifa na maendeleo ya jamii katika eneo la kusini mwa dunia, Afrika na haswa Tanzania. Wanazuoniwanaonyesha jinsi ambavyo udhibiti wa rasilimali za taifa uliendelea kukandamiza haki za wananchi hata baada ya uhuru. Ukiukwaji huo wa hakiunaendelea hata sasakwa njia tofauti huku udhibiti wa rasilimali za thamani ukiimarishwakuvutia hisia za utaiifa wakati pia maslahi ya kisiasa na ya kibinafsi ya ulimbikizaji wa mali, umashuhuri wa kisiasa n.k vikilindwa. Ni dhahiri kwamba sauti za wananchi zinazokosoa mwenendo huu hunyamazishwa hukumabadiliko katika sera yakiendelea kutoa mamlaka makubwa kwa serikali ikiwa ni pamoja na upanuzi wa maeneo ya uhifadhi unaoendelea kuchukua ardhiba wananchi. Hivi karibuni, ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za uhifadhi umekuwa ndio namna ambayo upanuzi wa hifadhi umefanikiwa sana. Ukandamizaji umetokea kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja matukio ya vitisho kwa wamiliki wa asili wa rasilimali. Hata hivyo, wanazuoni hawajajadili mambo haya waziwazi ili kushawishi mabadiliko ya sera za maendeleo ya jamii kusini mwa dunia. Mhadhara huu unatoa fursa ya kujadili mambo haya.

Mhadhara huu ni sehemu ya Kongamano la Kimataifa la Voice of Social Sciences (VSS) 2024.

# RATIBA YA MHADHARA

## MUSTAKABALI WA MALIASILI NA HAKI ZA BINADAMU NCHINI TANZANIA

Tarehe: 6 Novemba 2024

Ukumbi: Old Council Chamber

| Muda                  | Tukio                                     | Muhusika             |
|-----------------------|---|----------------------|
| 8:00 – 8:10<br>Mchana | Kukaribisha wageni na maelezo juu ya Mada | Dr. Ng'wanza Kamata  |
| 8:10 – 8:15<br>Mchana | Utambulisho wa Mhadhiri                   | Prof. Christine Noe  |
| 8:15 – 9:00<br>Mchana | Mhadhiri kuzungumza                       | Prof. Emmanuel Sulle |
| 9:00 – 10:30<br>Jioni | Mjadala                                   | Wote                 |





**UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM**  
**COLLEGE OF SOCIAL SCIENCES (CoSS)**

**VOICE OF SOCIAL SCIENCES (VSS2024)**  
**INTERNATIONAL CONFERENCE**



**AFRICA IN THE AGE OF UNCERTAINTIES:**  
**RISKS, RESILIENCE AND FUTURE**  
**PROSPECTS**



*University of Dar es Salaam*